**HALMASHAURI YA WILAYA YA BARIADI**

**MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI TAREHE 25/11/2021.**

---

**MAHUDHURIO YA WAJUMBE:**

1. HAMIS SHOLOLO - Mwenyekiti
2. FIDELI F. M - Katibu
3. ENG. W. S. MAKALA - Mjumbe
4. NOEL SHAMAZUNGU - Mjumbe
5. JOSEPH BALELE - Mjumbe
6. RAYMOND M. COSMAS - Mjumbe

**AGENDA ZA KIKAO:**

1. Kufungua Kikao
2. Kuridhia agenda ya kikao
3. Kuridhia kutumia njia ya nguvu ngazi (force account)
4. Kuahirisha kikao

**AGENDA NA. 01/25/11/2021 KUFUNGUA KIKAO:**

Mwenyekiti alifungua kikao kwa kuwakaribisha wajumbe kwenye kikao na kuwaomba kupitia kwa umakini wongozo wa Wizara kuhusiana na njia ya kutumia katika kutekeleza miradi ya UVICO -19, katika ujenzi wa madarasa, kwa shule za msingi, sekondari na majengo ya afya.Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa nne asubuhi.

**AGENDA NA: 02/25/11/2021 KURIDHIA AGENDA YA KIKAO**

Wajumbe wameridhia agenda moja (1) kama ilivyowasilishwa

**AGENDA NA. 03/25/11/2021 KURIDHIA KUTUMIA NJIA YA NGUVU KAZI (FORCE ACCOUNT)**

Katibu wa bodi ya Zabuni alielezea kwamba Wizara imetuma mwongozo mwezi wa 11/2021 unaolezea kutumia njia ya nguvu kazi (force account) katika kutekeleza miradi ya ujenzi wa madarasa ya sekondari arobaini na nne (44) yenye thamani ya shilingi milioni mia nane themanini (Tsh. 880,000,000/=) na ujenzi wa shule za msingi shikizi madarasa ishirini na mbili (22) yenye

CamScanner

thamani ya shilingi milioni mia nne arobaini (Tsh. 440,000,000/=) pamoja na uijenzi wa majengo ya afya yenye thamani ya shilingi milioni mia tatu tisini (Tsh.390,000,000/=), jengo la watumishi wa afya Tsh. 90,000,000/= na jengo la Dharura (EMD) Tsh. 300,000,000/=

Katibu wa Bodi ya zabuni alieleza njia hii inasaidia kupunguza gharama za ujenzi kwa kuwa inatumia local fundi, pamoja na kushirikisha jamii wanaozunguka mradi na kupelekea jamii kujipatia kipato, wajumbe wameridhia njia hiyo ya nguvu kazi (force account) kwa kuwa ina manufaa kwa jamii wanaozunguka mradi.

**AGENDA NA. 03/25/01/2021 KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kuhudhuria kikao kwa wakati na kwa michango yao mizuri, Mwenyekiti ameahirisha kikao mnamo saa kumi na nusu Alasiri.

**Muhtasari huu umethibitishwa:**

Tarehe 25.11.2021

Saini ....................

Jina Hamis Sitoloro

**MWENYEKITI**

Tarehe 25/11/2021

Saini ....................

Jina FIDELI F. M.

**KATIBU**

CamScanner

# MAHUDHURIO YA WAJUMBE BODI YA ZABUNI KWENYE KIKAO CHA KURIDHIA NJIA YA KUTEKELEZA MRADI

TAREHE 25/11/2021.

| | JINA KAMILI | WADHIFA | MUDA | SAHIHI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | HAMIS SHOLOLO | M/KITI | 9:30 | |
| 2. | FIDELI F. M | KATIBU | 9:30 | |
| 3. | Eng. W. S. MAKALA | MJUMBE | 9:30 | |
| 4. | Noel Shamanga | Mjumbe | 9:30 | |
| 5. | Joseph Balele | Mjumbe | 9:30 | |
| 6. | Raymond. M. Cosmas. | Mjumbe | 9:30 | |